## Kusoma Zaidi

# Maelezo kuhusu aina za kusoma.

- **Kusoma kwa ufahamu-** Hii ni mbinu ya kusoma matini, kung'amua matini kwa lengo la kuelewa unachosoma kwa kuzingatia maneno na sentensi.
- **Kusoma kwa ufasaha –** Ni kuwa na uwezo wa kusoma matini kwa kuzingatia vipengele vya usomaji wa ufasaha kama kasi ifaayo, matamshi bora, kiimbo, matumizi ya ishara.
- **Kusoma kwa kina –** Mbinu ya kusoma matini kwa makini zaidi na kwa nia fulani kama kwa mfano; kujibu maswali, kuchambua wahusika, maudhui na dhamira.
- **Kusoma kwa mapana –** Usomaji unaohusu kusoma matini mbalimbali kwa mpana ili kukuza stadi ya kusoma.
- **Kusoma kwa kurabaza/ Kusoma kwa kulenga dhana/wazo muhimu –** Kusoma matini kunakoelekezwa na nia ya kupata kuu katika matini.
- **Kusoma kwa Kurashia/kusoma upitiaji upesi –** Kusoma kunakoongozwa na lengo la kupitia matini kijuujuu ili kupata habari kimsingi.